JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO**

Telegram **"AFYA", DODOMA**
Nambari ya Simu: **+255 026 – 2323267**
E- Mail Na. ps@afya.go.tz

Mji wa Serikali Mtumba,
Barabara ya Afya,
S.L. P 743,
4**0478 DODOMA.**

## TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

## TAARIFA YA MWENENDO WA UGONJWA WA CORONA (COVID-19) NCHINI

**Dar es Salaam, Jumatatu Aprili 06, 2020**

Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto inathibitisha kuwepo kwa kesi mpya Nne (4) za maambukizi ya virusi vya corona (COVID- 19) zilizopatikana Dar es Salaam, Mwanza na Zanzibar na kufanya kuwepo kwa jumla ya kesi 24 zilizoripotiwa tangu kuanza kwa ugonjwa huu nchini. Wagonjwa hawa ni pamoja na wagonjwa wawili(2) ambao wametolewa taarifa na Waziri wa Afya wa Zanzibar tarehe 5/4/2020.

Wagonjwa wapya wawili (2) wa Tanzania Bara ni mwanaume mwenye umri wa miaka (41) raia wa Tanzania, mfanyabiashara mkazi wa Mwanza aliyeingia nchini kutoka Dubai tarehe 24 Machi, 2020 kupitia uwanja wa ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA) na kuelekea Mwanza tarehe 29, Machi 2020 ambapo alichukuliwa vipimo na kukutwa na maambukizi ya virusi vya corona.

Mgonjwa mwingine ni mwanaume mwenye umri wa miaka 35 raia wa Tanzania, mkazi wa Dar es Salaam, mfanyabiashara.

Wagonjwa wote wako chini ya uangalizi wa watoa huduma za afya katika vituo maalum vya tiba Dar es Salaam, Zanzibar na Mwanza. Wizara ya Afya inaendelea kuwafuatilia watu wa karibu (contacts) waliowahi kukutana na watu hao ili kudhibiti maambukizi mapya nchini.

Serikali inatoa msisitizo kwa wananchi kuzingatia maelekezo ya wataalam wa afya ya kujikinga na maambukizi ya virusi vya Corona (COVID- 19) hususan kwa kunawa mikono kwa sabuni na maji tiririka. Aidha, tunawasisitiza wananchi pia kuzingatia maelekezo mengine yanayohusu kuepuka mikusanyiko isiyo ya lazima na kukaa umbali usiopungua mita moja kati ya mtu na mtu.

Ummy A. Mwalimu (Mb)

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO**